# DAVID MASSAMBA: MWANAISIMU MWENYE HAZINA FICHE KATIKA FASIHI YA KISWAHILI

**Issaya Lupogo[1] & Hassan R. Hassan[2]**

[1]Chuo Kikuu Mzumbe – islupogo@mzumbe.ac.tz
[2]Chuo Kikuu cha Dodoma – hassan.hassan3@udom.ac.tz

**Ikisiri**

*Watu wengi wanamfahamu Hayati Prof. David Massamba kama mwanazuoni aliyemakinikia uga wa isimu kwa kiwango kikubwa huku baadhi ya vitabu vyake vikiwa maarufu katika ulimwengu wa Kiswahili. Hata hivyo, lipo jambo ambalo watu wengi hawalijui kwa mwanazuoni huyu; nalo ni suala la kujikita kwake katika kuandika kazi za kifasihi, hususani uga wa ushairi. Kwa hiyo, lengo la makala hii ni kubainisha na kuelezea hazina iliyojificha ya Massamba ili watu wapate kuijua na kuitumia kama ambavyo wanatumia maarifa yake ya isimu. Makala hii ni matokeo ya utafiti wa maktabani ambapo waandishi wametalii kazi mbalimbali za Massamba katika isimu na fasihi. Data zimechanganuliwa kwa kutumia mkabala wa kitaamuli chini ya Nadharia ya Uwasifu. Imebainika kwamba Massamba ana hazina fiche katika fasihi hususani katika ushairi wa Kiswahili ambapo ameandika Diwani ya Massamba na makala ya kinadharia inayohusiana na utunzi wa ushairi wa Kiswahili. Makala hii imejaribu kutoa muhtasari wa kazi hizo ili kuwahamasisha watu kusoma na kujipatia maarifa yaliyomo katika kazi hizo za kifasihi za Massamba.*

**Dhana za Msingi**: Mwanaisimu, Hazina Fiche, Utunzi wa Ushairi, Diwani

## 1.0 Utangulizi

Marehemu David Massamba ni mwanataaluma maarufu katika ulimwengu wa Kiswahili aliyejulikana sana katika uga wa isimu ya Kiswahili hasa katika fonolojia; watu wengi hawajui kuwa mwanazuoni huyu alijihusisha na fasihi pia kama ambavyo itadadavuliwa vema katika vipengele vya mbele katika makala hii. Sehemu hii ya utangulizi inaeleza taarifa za msingi za mwanazuoni huyu ikiwamo kuzaliwa na kufariki, safari yake ya elimu, na kazi zake za kitaaluma kwa ujumla.

Katika kitabu cha *Diwani ya Massamba*, sehemu ya maelezo kuhusu mwandishi, imeelezwa kwamba David Massamba alizaliwa mwaka 1945 katika Kijiji cha Kurwaki kilichopo katika kata ya Mugango, wilayani Musoma. Alimaliza darasa la nne mwaka 1957 katika Shule ya Mennonite Mission. Akaendelea na darasa la tano mpaka la nane katika shule ya bweni ya Kasoma. Baada ya hapo, akachaguliwa kujiunga na masomo ya kidato cha nne mwaka 1965. Mwaka 1966 alipelekwa katika Chuo cha Ualimu Butimba ambako alihitimu mafunzo ya Ualimu Daraja la "A" mwaka 1977. Alianza kufundisha katika shule za msingi wilayani Singida mnamo Novemba 1967. Aliendelea na kazi hiyo ya ualimu mpaka Julai 1972 alipohamishiwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam katika Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili - TUKI (kwa sasa Taasisi ya Taaluma za Kiswahili - TATAKI) kama Mchunguzi Msaidizi. Julai 1973 alifaulu kuingia Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kusomea Shahada ya Awali ya Sanaa katika Ualimu na Elimu ya Watu Wazima kama mwanafunzi-mfanyakazi.

Pia, Kahigi (2023) kupitia kongandao (kongamano la mkondoni) la kumbukizi ya Hayati David Massamba lililofanyika tarehe 10 Septemba 2023 kuanzia saa 10:30 alasiri hadi saa 1:37 usiku kwa saa za Afrika Mashariki, alieleza historia ya mwanazuoni huyu ambaye alikuwa rafiki yake enzi za uhai wake wote. Kahigi aliongezea mambo kadhaa mbali na haya yaliyokwishaelezwa. Kahigi alianza kwa kueleza kwamba anamkumbuka Massamba kama mwanafunzi mwenzake, mfanyakazi mwenzake, mwanaisimu mwenzake, na msaka-maarifa mwenzake. Alibainisha kwamba Massamba alimaliza Shahada ya Umahiri katika Isimu katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kisha akajiunga na Shahada ya Uzamivu katika Chuo Kikuu cha Indiana, Marekeni. Aliongeza kwamba Massamba alijihusisha katika shughuli zifuatazo wakati yupo katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam:

(a) Semina za Kiswahili kuhusu ufundishaji wa Kiswahili sekondari zilizokuwa zikiendeshwa nchi nzima mwaka 2003-2004 na zilishirikisha Idara ya Kiswahili na TUKI;
(b) Mradi wa Lugha za Tanzania ambapo Massamba alikuwa Mhariri Mkuu wa machapisho ya makala;
(c) Uandaaji wa programu za Shahada ya Kwanza, Shahada ya Umahiri na Shahada ya Uzamivu katika taasisi mpya ya TATAKI (mwaka 2009); na

(d) Uandishi/Uhariri wa vitabu vya shule za msingi na sekondari, suala lililoratibiwa na Taasisi ya Elimu Tanzania.

Vilevile, Massamba alishawahi kushika nyadhifa mbalimbali wakati anafanya kazi Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ikiwamo kuwa Mkurugenzi wa Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI) kuanzia mwaka 1985 hadi 1991. Aidha, Massamba alikuwa Mwasisi na Mkurugenzi wa Kampuni ya Uchapaji na Uchapishaji ijulikanayo kwa jina la Kiswahili Development Limited; ambapo pamoja na mambo mengine alikuwa akichapisha makala za kitaaluma katika jarida lijulikanalo kwa jina la *Jarida la Kimataifa la Isimu ya Kibantu* (JAKIKI). Vilevile, Massamba anatajwa kuwa Mtanzania wa kwanza kuandika na kutoa mhadhara wa uzinduzi wa uprofesa kamili akiwa TATAKI, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Prof. David Massamba alifariki tarehe 27 Agosti 2023 na kazikwa tarehe 30 Agosti 2023 kijijini kwao Kurwaki, Musoma mkoani Mara.

Kama ambavyo imedokezwa awali, Massamba anajulikana sana katika uga wa isimu ya Kiswahili huku watu wengi hawajui kuwa mwanazuoni huyu alijihusisha na fasihi ya Kiswahili. Hivyo, makala hii inaangazia kwa mapana mchango wake katika Kiswahili kwa kuonesha yale aliyoyafanya katika isimu ya Kiswahili na yale aliyoyafanya katika fasihi ya Kiswahili, ambayo yanaonekana kujificha machoni mwa watu wengi. Masuala ya kifasihi yaliyojificha ndiyo yanayodhihirishwa na makala hii kuwa ni hazina fiche.

## 2.0 Methodolojia na Nadharia Iliyotumika

Utafiti uliozalisha makala hii ulitumia mkabala wa kitaamuli ambapo data zilichambuliwa kimaelezo. Data zilikusanywa maktabani kwa kupitia machapisho mbalimbali ya mwandishi David Massamba. Ukusanyaji na uchanganuzi wa data uliongozwa na Nadharia ya Uwasifu (*Biographical Theory*). Nadharia hii haina mwasisi mmoja bayana kutokana na sababu kwamba wanazuoni kadhaa wameshiriki kuchangia kuiibua na kuidadavua katika vipindi tofauti. Baadhi ya wanazuoni hao ni Leon Edel mwaka 1973 aliyemakinikia wasifu katika kazi za fasihi kwa kuangazia jinsi kazi za fasihi zinavyoathiriwa na maisha ya waandishi wake; na Giorgio Vasari mwaka 1998 aliyeandika wasifu kuhusu maisha ya wasanii.

Nadharia ya Uwasifu inahusu suala la kumwelezea mwandishi wa kazi fulani ili kupata msingi wa kazi yake kinagaubaga. Hii inajumuisha kuelewa tajiriba na maisha yake kwa ujumla, alama alizoziacha katika uga wake wa uandishi, pamoja na usuli wa masuala yake yoyote ya muhimu. Nadharia hii ina misingi mikuu mitatu: Mosi, kutambua dhamira ya mwandishi ili kuielewa kazi yake. Pili, kazi ya fasihi ichambuliwe kwa kuzingatia muktadha husika. Hii ina maana kwamba ni vema kuyafahamu mazingira ya kihistoria na kiutamaduni yanayomzunguka mwandishi yakiwamo masuala ya kiutamaduni, mila na desturi, hali ya kisiasa, pamoja na changamoto binafsi za mwandishi. Tatu, kazi ya fasihi inapaswa ioneshe uhusiano kati ya mwandishi na kazi yake. Msingi huu unaonesha uhusiano uliopo kati ya mwandishi na kazi yake; matahalani, kufahamu jinsi maisha ya mwandishi yanavyoweza kuathiri kazi yake. Kimsingi, nadharia hii ilikuwa ni mwafaka katika utafiti uliozalisha makala hii kwa sababu msingi wa uchambuzi wa data za makala umejikita katika kufafanua kazi zilizofanywa na mwandishi mmoja (Massamba). Uchambuzi umejikita katika kubainisha na kuweka wazi kazi alizozifanya katika nyuga mbalimbali za taaluma za Kiswahili. Hivyo, ni dhahiri mchakato huu unahusiana kabisa na Nadharia ya Uwasifu.

## 3.0 Matokeo na Mjadala

Sehemu hii inaonesha matokeo ya uchanganuzi wa data za maktabani ambapo matokeo hayo yamegawanyika katika vipengele viwili: Mosi, kumwonesha Massamba kama mwanaisimu. Pili, kuelezea hazina fiche ya Massamba katika uga wa fasihi ya Kiswahili.

### 3.1 Massamba kama Mwanaisimu wa Kiswahili

Kama ambavyo imedokezwa katika utangulizi, Massamba ameandika machapisho mengi katika isimu, na ndio uga ambao alijipambanua nao kwa kiasi kikubwa. Kwa hiyo, sehemu hii inatumia Nadharia ya Uwasifu kubainisha alichokifanya Massamba katika isimu. Massamba ameandika makala mbalimbali za kitaaluma pamoja na vitabu ambapo machapisho hayo mengine kaandika peke yake na mengine kashirikiana na wanazuoni wengine. Baadhi ya wanazuoni alioshirikiana nao sana ni Yared Kihore na Yohana Msanjila. Vilevile, Massamba alikuwa mwalimu wa kozi za isimu kwa wanafunzi wanaosoma Shahada ya Awali, Umahiri na Uzamivu katika Kiswahili ikiwa ni pamoja na kusimamia tafiti mbalimbali za wanafunzi hususani wa Shahada ya Umahiri

na Uzamivu katika Kiswahili. Jedwali Na.1 linaonesha baadhi ya machapisho yake kwa upande wa vitabu katika nyuga mbalimbali ambapo mengi ameyaandika kwa lugha ya Kiswahili na machache amayeaandika kwa lugha ya Kiingereza.

Jedwali Na. 1: **Baadhi ya Vitabu Vilivyoandikwa na David Massamba**

| **Na.** | **Uga** | **Kitabu/Vitabu** |
|---|---|---|
| 1 | Istilahi | *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha* |
| 2 | Leksikografia ya Kiswahili | *a) Kamusi ya Isimu na Lugha*<br>b) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (Mwanajopo, matoleo kadhaa) |
| 3 | Lugha za Asili | *Kamusi ya Kiruri-Kiingereza-Kiswahili* |
| 4 | Historia ya Kiswahili | *a) Historia ya Kiswahili*<br>*b) Historia ya Kiswahili*: *Mtazamo Mpya 100KK hadi 2000BK*<br>c) *Kiswahili Origins and the Bantu Divergence-Convergence Theory* |
| 5 | Mofolojia | *Sarufi-Maumbo ya Kiswahili Sanifu* (SAMAKISA) (mwandishi mwenza) |
| 6 | Sintaksia | *Sarufi-Miundo ya Kiswahili Sanifu* (SAMIKISA) (mwandishi mwenza) |
| 7 | Isimu-jamii | *Isimu-jamii*: *Sekondari na Vyuo* (mwandishi mwenza) |
| 8 | Fonolojia | a) *Fonolojia ya Kiswahili Sanifu* (FOKISA)<br>*b) Phonological Theory*<br>*c) Maendeleo ya Nadharia ya Fonolojia*<br>d) *Misingi ya Fonolojia* |

**Chanzo:** Data za Maktabani (2024).

Aidha, makala hii haijadadavua kwa undani maudhui yaliyomo katika kazi mbalimbali za isimu za Massamba (kama zilivyooneshwa katika Jedwali Na. 1). Hii ni kwa sababu kazi hizo zinafahamika na watu wengi, na zinapatikana kirahisi; mathalani, vitabu hivi karibia vyote vinapatikana Chuo Kikuu cha Dar es Salaam katika Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (TATAKI). Makala hii inamakinikia kwa undani kazi za Massamba za fasihi (hazina fiche) ambazo watu wengi hawazijui kwa sababu hazikuwahi kuwa maarufu kama machapisho yake ya isimu.

### 3.2 Hazina Fiche ya Massamba katika Fasihi ya Kiswahili

Sehemu hii inajadili na kuweka wazi hazina fiche ya Massamba katika fasihi ya Kiswahili kwa kuongozwa na misingi mitatu ya Nadharia ya Uwasifu iliyoelezwa hapo awali. Kwa mujibu wa makala hii, hazina fiche ina maana ya maarifa ya Massamba ambayo kwa kiasi kikubwa watu wengi hawayafahamu. Kutofahamika huko kumetokana na jinsi Massamba alivyotambulika kwa wengi kama mwanaisimu kutokana na kufanya kazi nyingi za kitaaluma katika isimu ya Kiswahili. Utafiti uliozalisha makala hii umebaini kuwa zipo hazina fiche ambazo kimsingi zinapaswa kujulikana pia. Hazina fiche zilizobainika katika taaluma nje ya isimu ya Kiswahili ni mbili ambazo zinampambanua Massamba kama mwanafasihi kupitia utanzu wa ushairi wa Kiswahili. Hazina hizo ni kitabu cha mashairi kiitwacho *Diwani ya Massamba* na makala ijulikanayo kwa anwani ya *Utunzi wa Ushairi wa Kiswahili*.

#### 3.2.1 *Diwani ya Massamba* (1976)

Kihistoria, Afrika Mashariki imetokea kupatikana kwa watunzi mashuhuri wa sanaa ya ushairi wa Kiswahili. Hawa tunaweza kuwaona vizuri tukiiangazia historia ya ushairi wa Kiswahili. Miongoni mwa watunzi waliojipatia heshima kutokana na utungaji wa mashairi na kuusemea ushairi wa Kiswahili kinadharia na kivitendo ni David Massamba. Yeye ni mshairi maarufu wa Kiswahili wa karne ya 20. Ustadi wake katika sanaa hii unatiliwa mbolea na diwani yake ijulikanayo kwa jina la *Diwani ya Massamba*. Diwani hii yenye jumla ya tungo 36 imechapishwa mwaka 1976 na shirika la uchapichaji la Nelson Africa Ltd, Nairobi, Kenya. Kama ilivyo kawaida ya kazi za kifasihi, *Diwani ya Massamba* nayo inajitokeza ikiwa na dhati ya kuelimisha

na kuburudisha jamii. Katika sehemu inayofuata tumeeleza muhtasari wa fani na maudhui katika diwani hii kama vipengele muhimu katika kazi ya fasihi.

#### 3.2.1.1 Fani katika *Diwani ya Massamba*

Fani ni ufundi wa kisanaa anaoutumia mtunzi wa kazi ya fasihi kufikisha maudhui yake. Katika diwani hii, vipengele mbalimbali vya kifani vimezingatiwa kwa ustadi na umakini mkubwa. Miongoni mwa vipengele hivyo ni mtindo, muundo, na matumizi ya lugha. Kwa upande wa mtindo, *Diwani ya Massamba* imefuata mtindo wa kimapokeo unaozingatia kanuni za urari wa vina na mizani (Kezilahabi, 1978). Hii inadhihirishwa si tu ndani ya mashairi lakini hata kupitia msimamo wa mtunzi katika utangulizi wa diwani yake anaposema:

> Naamini kuwa wale wenye mahaba ya ushairi uambiwao kuwa ni wa ‘ki-mapokeo’ watafurahi kuona kwamba kitabu hiki kinaunga mkono juhudi zao. Hao sina la zaidi la kuwaeleza bali natumai kitabu hiki kitawaliwaza (uk. v)

Mtindo huu wa kimapokeo umetawala katika mashairi yote 36 yaliyomo ndani ya diwani hii. Uwezo wa kutunga mashairi kwa kufuata misingi ya kimapokeo unamtangaza bayana Massamba kuwa ni stadi wa fani hii.

Kwa upande wa muundo, diwani hii imetumia miundo changamani yaani mtunzi amechanganya miundo mbalimbali katika diwani yake. Hapa tunaweza kuona muundo wa tathlitha (mistari mitatu kila ubeti) katika mashairi kama “La Kuvunda Halina Ubani” (uk. 53), “Ardhi Mama wa Kila Kitu” (uk. 54) na “Utawala ni Dhima” (uk. 55). Mashairi mengi ndani ya diwani hii yametumia muundo wa tarbia (mistari minne kila ubeti) mfano shairi la “Walioleta Muungano” (uk. 3), “Umoja wa Afrika” (uk. 9), “Kweli” (uk. 21) kwa kutaja kwa uchache. Pia, muundo wa takhmisa (mistari mitano kila ubeti) umetumika kwa mashairi mawili ambayo ni “Saba Saba Kamilifu” (uk.59) na “Wazazi Msiwahini” (uk. 60). Aidha, diwani hii imekusanya tungo ambazo zipo katika muundo wa tenzi kama vile “Namshukuru Jalia” (uk.1), “Mpenzi Hupendeki” (uk.15), “Bwana na Bibi Harusi” (uk.17), “Nimechoka” (uk. 27) kwa kutaja kwa uchache

Kuhusu lugha, mshairi wetu, David Massamba ametumia lugha ya kishairi iliyo rahisi yenye kueleweka kwa wengi. Aidha, mtunzi ameweza kuinogesha kwa kuirashia viungo adhimu vya lugha kama vile methali, misemo, tamathali za semi na taswira.

#### 3.2.1.2 Maudhui katika *Diwani ya Massamba*

Maudhui ni jumla ya mambo yote yanayosemwa na mtunzi wa kazi ya fasihi katika kazi yake. Katika diwani hii, tunamsikia Massamba akipaza sauti kufichua, kuonya, kukemea, kushauri na kuelimisha jamii kuhusiana na masuala mbalimbali kama yafuatayo:

##### 3.2.1.2.1 Umuhimu wa Elimu

Katika jamii nyingi ulimwenguni suala la elimu linasisitizwa sana. Viongozi wa kada mbalimbali mfano wa dini na serikali wamekuwa wakipaza sauti kwa watu kushikilia elimu. Kazi ya kufundisha umuhimu wa elimu imefanywa vizuri na mshairi David Massamba kupitia diwani hii. Ndani ya *Diwani ya Massamba* tunakutana na shairi liitwalo “Elimu Haina Kikomo” (uk. 37) linalozungumzia suala hili. Katika beti zake mashairi anaeleza kuwa elimu ina manufaa makubwa. Hii ni kwa sababu mtu hujifunza fani nyingi ambazo huweza kumsaidia katika kuyaendesha maisha kama asemavyo katika ubeti wa tatu:

Kaya unapoachia, unaingia shuleni
Jama mkifikiria, kweli huko ni kazini
Hesabuni waingia, na kusoma nyingi fani
Elimu nawambieni, kwamba haina kikomo

Ubeti huo unasisitiza thamani ya elimu katika maisha ya mtu. Kwa hakika, mtu anayepata elimu huwa anajiongezea maarifa. Isitoshe, elimu chambilecho Massamba haina kikomo (mwisho). Kupitia shairi hili, jamii inafundishwa kuhusiana na kuzingatia elimu na umuhimu wake katika maisha ya kila siku. Aidha, shairi hili linashabihiana na misingi yote ya Nadharia ya Uwasifu. Hii ni kwa sababu suala la elimu limetawala maisha yote ya mwandishi enzi ya uhai wake. Hivyo, ni dhahiri kwamba shairi hili la elimu linasadifu maisha yote ya David Massamba.

#### 3.2.1.2.2 Umuhimu wa Kusema Kweli

Kuhusu suala la kusema kweli limeelezwa kinagaubaga ndani ya *Diwani ya Massamba*. Katika shairi liitwalo “Kweli” (uk. 21), Massamba anasisitiza kuhusu suala la kusema kweli na umuhimu wake katika maisha ya kila siku. Kimsingi, shairi hili limetumia bahari ya kikwamba ambayo neno moja hurudiwa kama kianzio cha kila mshororo katika shairi zima (Wamitila, 2006). Lengo la bahari hii ni kusisitiza jambo. Kwa mantiki hiyo, ndipo inaonekana katika shairi la “Kweli” neno “kweli” limefanyiwa takriri na kutumika kuwa ni kianzio cha mishororo yote. Kwa kufanya hivi, hapana shaka kuwa mshairi anataka kusisitiza na kuonesha thamani na umuhimu wa kusema kweli. Mshairi ameainisha faida mbalimbali za kusema kweli kama vile kupendwa na watu mfano ubeti wa tatu anasema:

> Kweli shika kila saa, hadi utapohitimu
> Kweli ina manufaa, jambo hili tufahamu
> Kweli ikisha kujaa, wapendwa na wanadamu
> Kweli kwako ni imamu, kinara wa kila saa

Kupitia ubeti huo inaelezwa kuwa moja ya faida ya kusema kweli ni kupendwa na watu. Pia, “kweli” ni kiongozi (imamu). Hakuishia hapo tu, faida ya “kweli” imeendelea kutajwa kama vile “kumuacha mtu huru” (ub. 4), “kupata haki” (ub. 2), “kupendwa na watu” (ub. 5). Pia, mshairi ameonesha madhara mbalimbali ya kutosema kweli kama vile “kuwa matatani’ (ub. 7), “kuchukiwa na watu na kukabiliwa na mikasa” (ub.10). Kulingana na Nadharia ya Uwasifu, ni lazima kazi ya fasihi ichambuliwe kwa kuzingatia muktadha husika. Hii ina maana kwamba ni vema kuyafahamu mazingira ya kihistoria na kiutamaduni yanayomzunguka mwandishi yakiwamo masuala ya kiutamaduni, mila na desturi, hali ya kisiasa, pamoja na changamoto binafsi za mwandishi. Kwa mujibu wa utafiti uliozalisha makala hii, “kweli” anayoisema na kuisisitiza Massamba katika diwani hii ndio “kweli” aliyoishi na kuisimamia katika maisha yake halisi. Hivyo, ni wazi kuwa muktadha wa maisha yake yalizungukwa na “kweli” ambayo tunaona akiisisitiza katika shairi lake.

#### 3.2.1.2.3 Kujiepusha na Utegemezi

Suala la utegemezi limeelezwa kwa kina kupitia *Diwani ya Massamba*. Mshairi ameonesha suala hili na madhara yake katika mashairi mbalimbali kama vile "Usitamani cha Ndugu" (uk.24). Katika shairi hili, mshairi anafundisha na kukataza kuhusiana na suala la utegemezi. Shairi hili limejengeka katika msingi wa ile methali maarufu ya Kiswahili isemayo kuwa, "Mtegemea cha ndugu hufa masikini". Massamba amelionesha suala hilo huku akiitoa mifano mbalimbali na madhara ya kutegemea cha mtu kama asemavyo kwenye beti zifuatazo:

Mtumai cha nduguye, hufa ali masikini
Siyo mali yake yeye, japo ndugu yake nani
Hakuna ampataye, wote wanamweka chini
Ujumbe huu shikeni, cha ndugu usitamani

Yeye nduguyo kwa damu, si kwa mali alonayo
Kusema yako vigumu, jambo lahitaji moyo
Pata chako muadhamu, usingoje cha nduguyo
Chako nacho jivunie, cha ndugu usitamani

Kulingana na ubeti huo, ni wazi kuwa kila mtu katika jamii anahimizwa kujitegemea mwenyewe kwa kufanya kazi na kumiliki chake. Aidha, Massamba hakuishia katika kukataza utegemezi bali pia amefundisha njia mwafaka ya kuyamudu maisha. Katika ubeti wa sita anahimiza watu wajibidiishe katika kufanya kazi ili wajichumie mali kwa jasho lao. Kwa kufanya hivyo, kutasaidia kuondokana na ukunguni (utegemezi). Massamba anatongoa:

Fanya kazi kwa bidii, mali yako na upate
Ukunguni zima zii, mali yako utafute
Upate thawabu hii, 'siiache ikupite
Ujumbe huu shikeni, cha ndugu usitamani

Yanayosemwa katika ubeti huo ni waadhi mkubwa wa uzindushi kwa jamii. Hii ni kwa sababu kufanya kazi ni muhimu kwa mwanadamu na ni kipimo cha utu Aidha, suala linalojadiliwa katika shairi hili linahusiana na msingi wa tatu wa Nadharia ya Uwasifu ambao unasisitiza kazi

ya fasihi ioneshe uhusiano kati ya mwandishi na kazi yake. Hili linathibitika kupitia maisha ya Massamba ambapo enzi ya uhai wake alifanya kazi kwa bidii na kujiepusha na utegemezi. Hivyo, ni yakini kuwa njia mwafaka ya kuondokana na utegemezi ni kufanya kazi. Pia, wanajamii wanapaswa kuzingatia yasemwayo shairini ili kuepukana na madhara yaletwayo na utegemezi.

**3.2.1.2.4 Kuwathamini na Kuwaheshimu Wazazi**

Wazazi ni watu muhimu sana katika jamii. Kuwathamini na kuwaheshimu wazazi ni jambo linalosisitizwa ndani ya vitabu vya dini na kila mtu katika jamii. Massamba kama zao la jamii naye ameliona suala hili na kuamua kulipa umuhimu wake. Kupitia shairi la "Wazazi Msiwahini" (uk. 60) tunaona jinsi mafunzo yakitolewa kwa jamii kuhusiana na thamani ya wazazi. Mwandishi anaonesha wazi kuwa wazazi ndio chanzo cha sisi kuwapo kwa maana kupitia wao ndio sisi tumezaliwa. Anashauri na kuhimiza kuwaheshimu, kuwatendea wema, kuwapenda, kuwajali na kuwasaidia ili kupata baraka duniani. Ubeti wa pili Massamba anasema:

Wazazi msiwahini, mkazipata laana
Heshima zao wapeni, hivyo nao 'tapendana
Muwe mukiwaauni, kila pa kuwezekana
Siwatupe majaani, kumbukeni nyiye wana
Msizikose baraka, kwa wazazi kupingana

Somo linalotolewa kupitia beti za shairi hili lina tija kwa kizazi kilichopita, kilichopo na kijacho. Hii ni kwa sababu taasisi ya wazazi ni taasisi muhimu na nyeti inayopaswa kuheshimiwa muda wote. Haifai kwa watoto kuwatendea hiana wazazi wao kwa kuwavunjia heshima. Mshairi anaonesha kazi kubwa aliyoifanya mzazi kwa mtoto tangu kuzaliwa kwake mpaka kufikia hatua ya mtoto kujitambua. Kwa hakika wazazi wanastahili na kustahiki kuenziwa kwani wema wao daima haumithiliki na haulipiki.

**3.2.1.2.5 Kuchunga Ulimi**

Ulimi ni kiungo kilichopo ndani ya kinywa cha binadamu au mnyama. Kiungo hiki aghalabu ndicho kinachotumika kuonja, kuzungumza na kuramba (TUKI, 2019). Katika utungo uliotumia bahari ya utenzi na kupewa jina la "Johari za Dunia" (uk. 62) mshairi anafundisha suala la

kuhifadhi ulimi. Anaonesha wazi kuwa ulimi ni kiungo kidogo ambacho kinahitaji uangalizi mkubwa wakati wa kukitumia. Hivyo, tahadhari inatakiwa mno ili mtu asije akaponzeka na kuingia matatizoni kwa sababu ya ulimi. Mshairi anasema:

> Ulimi ni wa kuponza
> Uachapo kuutunza
> Nikwambayo baba tunza
> Tena sana shikilia

Katika ubeti huo, mshairi anahimiza kuhusu kutunza ulimi hasa wakati wa kuongea. Ulimi ukitumiwa vizuri basi mtu hupendwa na wengi kutokana na kauli njema. Pia, ukitumiwa vibaya, mwenye kuutumia watu humchukia. Massamba anashadidia hili kuanzia ubeti wa 11-14:

> Watu wote 'takusifu
> Kauli kiwa nadhifu
> Na uwapo mpujufu
> Wengi watakuchukia
>
> Ulimi wenye nasaha
> 'Takuweka mwenye raha
> Utaondosha karaha
> Amani utavutia
> Lakini wenye nazaa
> Utazileta fazaa
> Utapatwa na mawaa
> Mwana wangu nisikia

Kwa hakika, beti hizo zinatoa elimu kubwa yenye usia ndani yake kuhusiana na kuutumia vema ulimi. Usia kama huu wa kutumia vema ulimi umewashughulisha washairi wengi wa Kiswahili. Mathalani, katika *Utenzi wa Mwanakupona*, suala la kuchunga ulimi limesisitizwa. Mwanakupona anamuusia binti yake kwa kusema:

> Pili uwe na adabu
> Na ulimi wa thawabu
> Uwe mtu mahabubu
> Kula utakapongia
>
> (Mulokozi, 1999:125)

Katika ubeti huo, Mwanakupona anamnasihi binti yake kuwa na ulimi wenye thawabu yaani ulimi wenye kauli njema. Naye Shaaban Robert hakuacha kutia neno kuhusu ulimi kama asemavyo katika ubeti ufuatao:

Ulimi sio mkono
Si silaha vilevile,
Ulimi ni nyama nono
Utumie polepole,
Mchaguzi wa maneno
Na kusema kwa upole,
Huepuka magombano
Wala hajuti milele.

(Robert, 1973:30)

Beti hizo ni ithibati ya wazi kuwa kiungo cha ulimi kinapaswa kutumiwa kwa uangalifu mkubwa. Suala la matumizi mazuri ya ulimi katika maisha halisi ya Massamba yanadhihirika wazi. Hili linaafikiana na msingi wa tatu wa Nadharia ya Uwasifu unaosisitiza uhusiano wa fasihi na maisha halisi ya mtunzi. Utafiti uliozalisha makala hii ulibaini kuwa Massamba aliishi vizuri na watu kwa kuwaheshimu bila kuwatweza. Aidha, alikuwa fasaha wa uneni ambapo alitambua madhara yatokanayo na ulimi. Hivyo, alihakikisha anautumia ulimi wake kujenga na sio kubomoa kama anavyosisitiza katika utungo uitwao "Johari za Dunia" (uk. 62).

#### 3.2.1.2.6 Umuhimu wa Kukumbuka Wema

Wema ni matendo mazuri ambayo aghalabu hutokana na ukarimu. Wema ni hazina bora na wema hauozi. Katika maisha ya kila siku, watu wamekuwa wakitenda na kutendewa mema. Wema katika jamii ni kitu kikubwa sana ambacho huthaminiwa na wengi. Pia, kuna baadhi ya watu ni wepesi wa kusahau wema wanaotendewa na wengine hapa ulimwenguni. Hili linaelezwa kinagaubaga ndani ya *Diwani ya Massamba*. Katika shairi la "Usiache Mbachao" (uk. 50) mshairi anahimiza kuhusiana na kuthamini wema anaotendewa mtu hata kama utakuwa umepita miaka mingi. Kuthamini wema kunaijenga jamii na kuiweka katika hali ya kupendana na amani. Mshairi anakemea tabia ya kuutupa wema kutokana na kupata nafasi au cheo. Anawataka watu katika jamii wawe na kumbukumbu ya mema wanayofanyiwa. Katika ubeti wa kwanza na wa pili mshairi anasema:

Mbacha ‘siache wewe, kwa msala upitao
Kuukuu la mwenyewe, kuwa nalo angalao
Ulifanye ni mwenyewe, kila muda upitao
Usiache mbachao, kwa msala upitao

Upatapo hicho kipya, na akiba haiozi
Ni ya maana hedaya, ‘siione upuuzi
Kipya ‘takuwa hekaya, itapopita miezi
Usiache mbachao, kwa msala upitao

Beti hizo ni ithibati kuwa wema si kitu cha kukisahau. Mshairi anatumia kibwagizo cha methali maarufu ya Kiswahili ili kuifumbata hekima iliyomo ndani yake. Sambamba na hili, shairi hili ni moja ya mashairi ambayo yameathiriwa na maisha ya mwandishi David Massamba. Kimsingi, hoja hii inaenda sambamba na moja ya msingi wa Nadharia ya Uwasifu unaohusu uhusiano kati ya mwandishi na kazi yake. Kwa kuwa waandishi wa makala hii walikuwa wanayaona maisha ya Massamba; ni dhahiri kwamba alikuwa mtu mwema na mpenda watu daima. Hivyo, shairi hili linasadifu kabisa aina ya maisha yake.

**3.2.1.2.7 Adabu na Utii**

Adabu na utii ni miongoni mwa mambo yanayohimizwa sana katika jamii. Watoto wamekuwa wakihamasishwa na kufunzwa adabu na utii kwa waliowazidi rika. *Diwani ya Massamba* nayo haipo nyuma katika kulishughulikia hili kwani imefundisha kuhusiana na kuwa na utii na adabu. Mwandishi anaonesha kuwa adabu na heshima ni vitu muhimu mtu kuwa navyo. Vilevile, si vizuri kwa mtu kushika mwendo wa kiburi na ujeuri na kushindana na wakubwa. Haya tunayaona katika utenzi wa “Johari za Dunia” (uk. 62) kuanzia ubeti wa 17 - 22 mshairi anatuambia:

Adabu nayo heshima
Ni la tatu nalisema
Kwa yeyote vya lazima
Kuvikosa ni hatia

Uwapo kwenye kaumu
‘Sijifanye kichwa ngumu
Sana mno jiheshimu
Mbele yao nyenyekea

Kiburi si maungwana
Nacho sana epukana
Wakubwawo kushindana
Ni matata watakia

Waheshimu na wadogo
‘Siuone ni mzigo
Wala ‘sifanye mikogo
Mbele yao kuringia

Adabu njema ni kito
Kama utaishikato
‘Takuvusha kwenye mito
Uwezamo tumbukia

Beti hizo ni ushahidi wa jinsi suala la utii na adabu linavyofundishwa na kuhimizwa ndani ya *Diwani ya Massamba*. Mshairi anaonesha thamani ya adabu njema kuwa ni sawa na kito ambacho kila mtu anapaswa akishike kwa uangalifu ili asije kupotea. Pia, adabu na utii umehimizwa kwa kila mtu yaani wakubwa na wadogo. Maelezo yaliyomo ndani ya shairi hili yanaumana na msingi wa Nadharia ya Uwasifu unaohusu uhusiano kati ya mwandishi na kazi yake. Hii ni kwa sababu katika enzi ya uhai wake, Massamba alikuwa ni mtu aliyewatii wakubwa kwa wadogo. Hakuwa mtu mwenye kujikweza wala kuwavunjia adabu wenzake.

### 3.2.2 Makala ya “Utunzi wa Ushairi wa Kiswahili”

“Utunzi wa Ushairi wa Kiswahili” ni makala iliyoandikwa na David Massamba na kuchapishwa na TUKI mwaka 1983. Mwendelezo wa utunzi wa kazi za fasihi kwa Massamba ni udhihirisho tosha kwamba ijapokuwa alikuwa amejikita zaidi katika isimu, bado ndani yake alikuwa na kipaji cha sanaa ya fasihi; jambo ambalo ilibidi lijichomoze katika kazi yake. Hii ndio hali ya mwandishi inavyoweza kuathiri kazi yake, suala ambalo ni moja ya msingi wa Nandharia ya Uwasifu.

Makala hii ya “Utunzi wa Ushairi wa Kiswahili” ni miongoni mwa makala na rejea muhimu katika ushairi wa Kiswahili. Katika makala hii, Massamba anadhihirisha uweledi wake katika sanaa ya ushairi kinadharia. Hii ni kwa sababu ameweza kueleza mambo ya msingi yanayohusiana na ushairi wa Kiswahili kama anavyosema katika utangulizi wake kuwa “Madhumuni ya makala haya ni kuzijadili mbinu mbalimbali zitakikanazo katika utunzi wa

ushairi" (Massamba, 1983:54). Katika sehemu hii tutafanya mapito kwa muhtasari kuhusu mambo ya msingi anayoyaeleza Massamba ndani ya makala yake. Mambo hayo ni:

### 3.2.2.1 Dhana ya Ushairi

Sehemu ya kwanza ya makala ya "Utunzi wa Ushairi wa Kiswahili", inaanza kwa kutalii dhana ya ushairi. Ili kuweza kupata ufafanuzi mzuri wa suala hili, Massamba anazidondoa fasili mbalimbali za baadhi ya wataalamu wa taaluma hii ya ushairi wa Kiswahili. Mwandishi amezikusanya fasili za wataalamu wa ushairi wa kimapokeo kama vile Robert (1954), Mnyampala (1970) na Abdalla (1973). Anaeleza kuwa fasili hizo zina mawazo ya mshabaha mmoja kwa sababu ndani ya fasili zote kuna sifa chomozi zinazojitokeza katika ushairi wa Kiswahili. Wataalamu hao wanaafikiana kwamba mawazo mazito ni kitu muhimu sana katika ushairi wa Kiswahili. Aidha, mawazo hayo, maono na hisi za ndani lazima ziwe ndani ya sanaa maalumu ya vina, mizani, maneno ya mkato na lugha ya kunata. Baada ya kutalii fasili za wanamapokeo, pia anabainisha fasili za washairi wa kisasa. Hapa kazichambua fasili kama ya Topan (1973) na Kezilahabi (1973). Kupitia fasili zao, anabainisha kuwa hawakutupana sana na wataalamu wa mwanzo isipokuwa wanausasa hawakutilia mkazo suala la urari wa vina na mizani. Mwisho, Massamba anatoa hoja za muumano na mwachano wa fasili za wataalamu wa matapo hayo mawili na kuhitimisha kwa kutoa maoni yake kuhusiana na sanaa ya ushairi wa Kiswahili.

### 3.2.2.2 Tanzu za Ushairi

Katika kipengele hiki, Massamba anaonesha ustadi wake wa kuifahamu historia ya ushairi wa Kiswahili na mapito yake. Anaanza kwa kueleza kuwa chimbuko la ushairi ni nyimbo jambo ambalo limedhihirishwa na wataalamu mbalimbali wa ushairi wa Kiswahili akiwamo Abedi (1965); Shariff (1988), na Mulokozi (2017). Nyimbo zilizouchimbua ushairi wa Kiswahili zilikuwa zikiimbwa katika magoma ya harusi, pungwa, sherehe za jando na unyago, wakati wa kufanya kazi hasa za ushirikiano (Abedi, 1965; Chiraghdin na wenzake, 1975). Kwa mujibu wa Massamba (1983), maendeleo ya nyimbo hizo zilizaa tanzu mbalimbali kama vile tumbuizo, nyimbo, shairi, na tenzi. Tanzu zote hizo zimeelezwa kwa kirefu katika makala hiyo na kwa umahususi mkubwa akajadili utanzu wa tenzi, mashairi na ngonjera. Anaufafanua utenzi kuwa ni

utungo mrefu wa kishairi unaoeleza tukio au kisa fulani. Kwa kawaida, utenzi huwa na beti nyingi na mizani fupi. Ama kuhusu mashairi, amefasili na aina zake mbalimbali kama vile mashairi ya simango, mashairi ya kujigamba, mashairi ya uzindushi, mashairi ya kawaida, mashairi ya furaha, mashairi ya huzuni, mashairi mazito na mashairi ya kuadibu. Aina zote hizo anazisakafia kwa mifano madhubuti ya mashairi mbalimbali ili msomaji aweze kuelewa vizuri. Kwa upande wa ngonjera, Massamba anaeleza usuli wake na namna jamii inavyokanganyika kuhusiana na watu wengi kudhani kuwa ngonjera zilianzishwa na Mathias Mnyampala. Katika mkanganyiko huu, Massamba (1983) anaeleza kuwa Mnyampala si mwanzilishi wa ngonjera kwani ngonjera katika jamii ya Waswahili zilikuwapo tangu zamani kwa jina la "funga nyama". Hata hivyo, anakiri wazi kuwa katika utanzu wa ngonjera, Mathias Mnyampala ndiye Mtanzania aliyeuhuisha utanzu huu na kuasisi jina la ngonjera kutoka lugha ya Kigogo. Pia, aliweza kuandika vitabu viwili maarufu vya ngonjera ambavyo ni *Ngonjera za UKUTA 1* na *Ngonjera za UKUTA 2*.

**3.2.2.3 Mitindo ya Mashairi**

Kuhusu mitindo ya mashairi ya Kiswahili, Massamba aliitambua na kuibainisha kwa mifano ndani ya makala yake. Aidha, anaeleza wazi kuwa ushairi wa Kiswahili una mitindo mingi na si rahisi kusema kwamba kuna mitindo mingapi ya utungaji wa mashairi. Hii ni kwa sababu hutegemea sana ufundi wa mtungaji mwenyewe. Katika makala yake, Massamba anabainisha na kueleza mitindo mbalimbali ya mashairi ya Kiswahili kama vile mtindo wa pindu, mtindo wa msisitizo na mtindo wa beti kubadilishana vina. Mitindo mingine ni mtindo wa vina vya namna moja na mtindo wa kurudia mstari wa mwisho wa ubeti.

**3.2.2.4 Miundo ya Mashairi**

Kama ilivyo katika mitindo, mashairi pia yana miundo mbalimbali kutegemeana na ufundi wa mshairi mwenyewe. Massamba anaeleza kuwa ingawa kuna miundo mingi lakini kuna baadhi imezoeleka na kufahamika zaidi ya mingine. Anautaja muundo wa tarbia, ambao kila ubeti unakuwa na mistari minne kuwa ni muundo maarufu. Katika muundo huu, aghalabu huwa na mizani kumi na sita na mshororo unagawanyika katika vipande viwili vilivyo na mizani sawa (8+8). Muundo mwingine ni muundo wa tathnia ambao ubeti unakuwa na mistari miwili kila

ubeti. Muundo huu unatumika zaidi katika nyimbo. Muundo wa tathlitha (mistari mitatu kila ubeti) nao unatajwa sambamba na muundo wa takhmisa (mistari mitano kila ubeti) na muundo wa sablia (mistari saba kila ubeti).

**3.2.2.5 Umbo la Shairi**

Ni wazi kuwa katika usomi wake, Massamba aliufahamu ushairi wa Kiswahili na kutambua kuwa una umbo lake mahususi. Katika makala yake, anazungumzia umbo la shairi ambalo kimsingi linaundwa na vijenzi muhimu amabvyo ni vina, mizani, utoshelezi, muwala, mshororo na kipande. Licha ya kutambua umbo hilo na vijenzi vyake, pia anasisitiza kuwa umbo linaweza kubadilika sura kutegemeana na miundo mbalimbali na mitindo atakayotumia mshairi. Katika kusisitiza hili, anatoa mfano wa kitambaa cha nguo chenye vipimo maalumu katika pande zote, lakini kitambaa hicho kinaweza kubadilishwa sura kufuatana na mikunjo itakayotumiwa.

**3.2.2.6 Mtunzi wa Ushairi**

Katika sehemu hii Massamba anaeleza kunga za kuzingatia kwa mtunzi wa ushairi. Kwanza, anaanza kwa kuwagawa washairi katika matapo makubwa mawili ambayo ni: Washairi wanaoinukia na washairi wazoefu. Kwa matapo yote, Massamba anaeleza namna bora ya utunzi kifani na kimaudhui. Katika bahari ya maudhui, mtunzi wa mashairi anapaswa aijuwe falsafa yake katika maisha, falsafa ya jamii yake na hisia za watu wengine kuhusu falsafa yake. Aidha, anasisitiza kuwa mtunzi wa mashairi hatungi tu ila kwa haja. Hii ina maana kwamba lazima awe na jambo linalompa muwasho au mkereketo wa kutunga. Vilevile, katika maudhui ni lazima atunge kulingana na mambo yaliyomo katika jamii. Kwa upande wa fani, mtunzi anatakiwa kuzingatia vipengele muhimu vya kifani. Mathalani, katika mtindo, anamtaka mtunzi wa ushairi kujaribu kadiri awezavyo kuchagua na kutumia mtindo wa ushairi ambao anafikiri utakidhi zaidi haja ya dhamira yake. Pia, katika lugha lazima azingatie na kuwa makini sababu lugha ni kipengele muhimu sana katika ushairi. Hii ni kwa sababu lugha ya ushairi huwa ni teule, ya mkato na yenye kunata. Samababamba na hilo, lugha ya picha (taswira) nayo inasisitizwa katika kuleta uzuri na uhai wa shairi. Mtunzi atumie picha zenye kuleta athari kwa wasomaji wake kwa sababu lugha ya picha husaidia sana kuvuta hisia na kuleta mguso wa namna ya ajabu katika moyo wa msikilizaji au msomaji.

#### 3.2.2.7 Vina na Mizani

Hivi ni vipengele maarufu katika ushairi wa Kiswahili. Massamba (1983) anavifasili vipengele hivi na kuvielezea umuhimu wake katika shairi. Aidha, anafafanua vipengele vingine vinavyoungana na hivyo vya awali katika kulijenga shairi la Kiswahili. Vipengele hivyo ni kituo, muwala, ubeti, kipande na msisitizo. Mwisho, anasisitiza kuwa ushairi ni bahari pana na kila mtu anapaswa kuogelea kadiri ya uwezo wake.

## 4.0 Hitimisho

Kwa ujumla, David P.B Massamba ameacha alama kubwa sana katika taaluma za Kiswahili; si katika isimu tu, taaluma ambayo wengi wanamjua nayo na aliyojipambanua nayo zaidi, hata katika fasihi ya Kiswahili kupitia utanzu wa ushairi. Jambo linalompa upekee mwanazuoni huyu ni jinsi ambavyo kazi zake zimeweza pia kusawiri maisha yake halisi wakati wa uhai wake. Mathalani, mashairi mengi katika *Diwani ya Massamba* yanasadifu na kumulika mwenendo wa maisha ya mwandishi huyu; kama vile suala la kuzingatia elimu, na kuhimiza upendo, kuzingatia maadili na kuchunga kauli ili kutowakwaza watu wengine. Aidha, kuna mambo mengi ya kujifunza kutoka kwa Massamba ambapo kwa wanataaluma wa lugha ya Kiswahili wanakumbushwa kujituma katika kuandika na kuchapisha maarifa mbalimbali yanayokosekana katika Kiswahili. Wadau wengine wa Kiswahili wanakumbushwa kuendelea kusoma na kujifunza kupitia maandiko lukuki aliyotuachia mwalimu wetu, Massamba. Ijapokuwa Massamba amefariki, tunaendelea na tutaendelea kumsoma katika machapisho yake daima. Hii inaonesha wazi kwamba mtu mwenye elimu hai hufa mwili sio jina. Jina lake hudumu na kukumbukwa daima dawamu kama asemavyo Robert (1973:13) kuwa:

> Mtu mwenye elimu
> Wakati wa kufariki,
> Jina lake hudumu
> Milele kwa urafiki,
> Kwa kila hadithi tamu
> Aliyoacha sadiki,
> Atatunzwa na Karimu
> Pepo na kila haki
>
> Si la kupatwa na ufu
> Jina la mwenye elimu,

Hushindwa uharibifu
Kulifanya lisidumu,
Lina maisha marefu
Kuliko mwanaadamu,
Kitu hiki kitukufu
Moyo kifanyie hamu.

**Marejeleo**

Abedi, K.A. (1965). 'Utangulizi' katika Mnyampala, M. *Waadhi wa Ushairi*. Nairobi: East African Literature Bureau.

Chiraghdin, S., Nabhany, A. S., & Baruwa, A. (1975). *Tarehe ya ushairi wa Kiswahili*. *Mulika, 7*, 59–67.

Edel, L. (1973). *Literary Biography*. Indiana: Indiana University Press.

Kezilahabi, E. (1978). Diwani ya Massamba. *Mulika*, (13), 44–50.

Massamba, D.P.B. (1976). *Diwani ya Massamba*. Nairobi: Nelson Africa Ltd.

Massamba, D.P.B. (1983). Utunzi wa Ushairi wa Kiswahili. *Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili III*: *Fasihi*. Dar es Salaam: TUKI.

Mulokozi, M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: KAUTTU Limited.

Mulokozi, M. (1999). *Tenzi Tatu za Kale*. Dar es Salaam: TUKI.

Njogu, K. & Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi*: *Nadharia na Mbinu*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

Robert, S. (1973). *Tenzi za Marudi Mema na Omar Khayyam*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Shariff, I. N. (1988). *Tungo Zetu*. Trenton: The Red Sea Press Inc.

TUKI (2019). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press.

Wamitila, K. W. (2006). *Kamusi ya Ushairi*. Nairobi: Vide-Muwa.

Vasari, G. (1998). *The Lives of the Artists*. Oxford: Oxford University Press.